

**OFISI YA RAISI - TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

S.L.P363,  
TUKUYU,  
6/12/2020.

**KUMB: NA. KSS/ VOL . 31**

Jina la wanafunzi.....

S.L.P.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KINYALA  
WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

- 1.0** Ninafurahi kukuari fu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (01) katika shule hii mwaka 2021 muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shulenii tarehe 11/01/2021 saa moja asubuhi.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**2.1 SARE YA SHULE**

- (a) Sare ya shule (angalia kitambaa kilichoambatanishwa hapo juu) kwa wavulana - suruali na wasichana sketi na shati jeupe mikono mifupi na sare ya michezo ambazo ni kaptula na T- shirt ya njano kwa wanafunzi wa jinsi zote.
- (b) T-shirt kwa ajili ya kuvaliwa Alhamisi na ijumaa aje na Tshs, 12,000/= (zinapatikana shulenii).
- (c) Rangi ya Hijabu ni NYEUP.
- (d) Truck suit – DARK BLUE yenye mistari meupe pembeni.

**2.2 VIFAA**

- (i) Daftari kubwa kumi na mkebe wa hisabati.
- (ii) Kalamu.

**2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda na kurudi pamoja na matibabu ni gharama ya mzazi ( kikao cha wazazi kiliamua gharama za chakula ni shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa mwezi kwa wanafunzi wa kutwa, fedha hii anapaswa kuja nayo shule inapofunguliwa).**

**2.4 Wanafunzi anapaswa kuja na bunda moja la karatasi (ream) kwa ajili ya mitihani.**

**2.5 Wanafunzi anapofika aje na vifaa vya usafi wa mazingira jembe, kwanja na ufagio wa chelewa uliosukwa vizuri.**

**3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

- 3.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na.25yamwaka1978.Aidhainazingatiamiongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.**
- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.**

- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
- (d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyagine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (g) Kuвая sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

### **3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE:**

- 1) Uasherati, ubakaji na ushoga.
- 2) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- 3) Uvutaji bangi/ sigara.
- 4) Makosa ya jinai.
- 5) Kupigana au kupiga.
- 6) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- 7) Kudharau Bendera ya Taifa.
- 8) Kuoa au kuolewa.
- 9) Kupata mimba/ kusababisha mimba.
- 10) Kugoma au kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- 11) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- 12) Kumiliki au kupatikana na simu ya mkononi.

### **4. MAMBO MENGINE MUHIMU:**

- (a) Medical Examination form itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.  
Fomu hii utakabidhi kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulenii.
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki/ katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni za shule.
- (d) Leta kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

**“KARIBU KINYALA SEKONDARI”**

**“MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI KINYALA SEKONDARI”**

.....

**AMBEGE U.M  
MKUU WA SHULE**